# BRELA

## WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

ISSN: 0000401 | Toleo Na. 04 | Januari - Machi, 2023




# BRELA

## URASIMISHAJI BIASHARA WAONGEZEKA MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA

# YALIYOMO



BRELA YATOA UFADHILI WA MASOMO YA UZAMILI KATIKA FANI YA MILIKI UBUNIFU 4




WANAWAKE BRELA WAJIZOLEA SIFA KWA UCHAPAKAZI 5



TEKELEZENI KANUNI ZA WAMILIKI MANUFAA - HOMERA 6

13 URASIMISHAJI BIASHARA WAONGEZEKA MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA



## TAHARIRI

# Ujumbe wa Afisa Mtendaji Mkuu



*Bw. Godfrey Nyaisa*
*Afisa Mtendaji Mkuu BRELA*

Nafurahi kuwasilisha toleo la nne la jarida hili ambalo ni mwendelezo wa majarida mengine matatu ya awali. Jarida hili limesheheni taarifa na maelezo ya mafanikio na maboresho yanayofanywa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) katika kuuhabarisha umma mafaniko na changamoto za kiutendaji tunazokabiliana nazo. Lengo kuu likiwa ni kuweka mazingira bora na wezeshi ya kibiashara nchini.

Miongoni mwa mambo yaliyomo katika jarida hili ni mafanikio ya utekelezaji wa shughuli za BRELA katika miaka miwili ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Pia, kuna taarifa za jitihada zilizofanywa na BRELA katika kuboresha utoaji wa huduma za usajili na ulinzi ili kwenda sambamba na ofisi nyingine za kikanda na kimataifa zinazotoa huduma za usajili na ulinzi.

Kwa kuwa rasilimali watu ni nyenzo muhimu kwenye utendaji kazi BRELA imekuwa ikiwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwawezesha kushiriki mafunzo semina na warsha mbalimbali, ili waweze kutoa huduma bora kwa kuzingatia sheria, Kanuni na miongozo pamoja na Mkataba wa Huduma kwa Wateja (Client Service Charter).

Maendeleo ya dunia ya leo kwa kiasi kikubwa yanachangiwa na sayansi na teknolojia ambazo lazima zilindwe kisheria. Kwenye eneo hili BRELA imetoa ufadhili kwa wanafunzi wa shahada ya uzamili katika fani ya Miliki Ubunifu (Masters of Intellectual Property- MIP) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Tanzania bado ina uhitaji wa wataalamu wengi kwenye fani hii na BRELA itaendelea kutoa ufadhili kwenye mwaka ujao wa fedha.

Katika kuongeza ufanisi, weledi, tija na uwazi, BRELA imeendelea kutoa elimu na huduma saidizi kwa wadau hususan kwenye eneo la Hataza na maeneo mengine ya kulinda vumbuzi. Huduma hizi saidizi ni pamoja na kutoa elimu na mafunzo ya umuhimu wa kurasimisha biashara nchini.

Sambamba na kujenga uwezo kwa watumishi na wadau wa BRELA, pia jarida hili limeangazia masuala ya uwajibikaji na uwazi katika utoaji wa huduma. Wakala imetoa elimu ya udhibiti wa utakatishaji fedha kwa vyombo vya uchunguzi na elimu kwa wamiliki wa kampuni kuhusu utekelezaji wa kanuni za Wamiliki Manufaa (Beneficial Ownership).

Kwa ujumla habari zilizomo katika jarida hili zimebeba taarifa za utekelezaji wa shughuli na majukumu ya BRELA kupitia idara na vitengo, yakiwemo mafunzo maalumu ya uongozi kwa watumishi wanawake, elimu ya sheria na mikataba ya kimataifa inayolinda ubunifu katika programu za kompyuta ili kurahisisha utoaji wa Hataza kwa waombaji.

BRELA itaendelea kuboresha huduma zake kwa kuwa mlango wa kwanza wa urasimishaji biashara na kichocheo kwa ujio wa wawekezaji nchini. Kwa mantiki hiyo, BRELA tunaendelea kujenga uelewa wa pamoja kwa wadau mbalimbali nchini. Hii ni kwa ajili ya kuwezesha ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa huduma bora katika kujenga mazingira wezeshi ya kibiashara nchini.

Lengo letu kubwa ni kuipa biashara yako uhai wa kisheria kupitia urasimishaji. Ni matarajio yangu makubwa kuwa utafurahia jarida hili na pia utajifunza mengi.

## BODI YA UHARIRI

**Andrew Mkapa**
**Mwenyekiti**

**Wajumbe**

Meinrad Rweyemamu
Tawi Kilumile
Abdulrahman Songoro
Neema Kitala
Tulizo Mpina
Alpha Nuhu

**Roida Andusamile**
**Katibu**

# BRELA yatoa ufadhili wa masomo ya uzamili katika fani ya Miliki Ubunifu




*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa (wa pili kulia) akimkabidhi mfano wa hundi Bw. Stanslaus Kigosi ambaye amepata ufadhili wa masomo ya Shahada ya Uzamili ya Miliki Ubunifu.*

**Na Njwaba Mwaijibe**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imetoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi watano ambao wanasoma Shahada ya Uzamili katika fani ya Miliki Ubunifu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Akikabidhi hundi hizo za ufadhili Machi 10, 2023 Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw. Godfrey Nyaisa alisema kuwa BRELA inafanya kila jitihada kuhakikisha watalaamu wanaongezeka na elimu ya Miliki Ubunifu inawafikia watu wengi zaidi.

Aliongeza kuwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wamefanikisha kuwepo kwa mafunzo hayo ya Miliki Ubunifu ambayo kwa kiasi kikubwa yataongeza uelewa na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

"Ndugu Waandishi wa Habari tumetoa ufadhili huu kwa kuzingatia jinsia na makundi maalum na kwa awamu hii tumefadhili wanafunzi watano na kiasi cha Shilingi Milioni Kumi na Sita Laki Tano na Elfu Hamsini (16,550,000/=) Kimetolewa", alisema Bw. Nyaisa.

Aliwataja wanafunzi hao waliopata ufadhili kuwa ni pamoja na Bi. Grace Ezekiel Mwaikono kutoka Mahakama Kuu, Bw. Stanslaus Aidan Kigosi kutoka BRELA, Bw. Addo November Mwasongwe kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Bw. Eric Maximillian Mlasani kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Bi. Merciana Nehemiah Ntabaye kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Vilevile, alitaja lengo la ufadhili kwa wanafunzi hao kuwa ni kupanua wigo wa utaalamu katika nyanja ya Miliki Ubunifu kwakuwa eneo hilo muhimu halina wataalamu wengi hapa nchini, kuongeza ufahamu kuhusu Miliki Ubunifu kwa maendeleo chanya ya Taifa la Tanzania kutokana na umuhimu wake katika maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Aliongeza kuwa ufadhili huo utahamasisha wanufaika kutambua faida zinazopatikana kutokana na elimu kuhusu Miliki Ubunifu na jinsi ya kuitumia katika kuendeleza na kukuza Ubunifu nchini, kuweka mkazo mahsusi katika muunganisho wa sheria na sera za Miliki Ubunifu katika muktadha wa mienendo iliyopo ya kiuchumi na kijamii inayopatikana barani Afrika.

Kwa upande wake Dkt. Sosthenes Materu, ambaye ni Amidi wa Shule Kuu ya Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliwashukuru BRELA kwa ufadhili huo sambamba na jitihada za Taasisi hiyo katika kuendeleza Miliki Ubunifu kwa ajili ya kuchochea maendeleo.

Mwakilishi wa wanufaika wa ufadhili wa BRELA ambaye ametoka katika kundi la watu wenye mahitaji maalumu Bw. Erick Maximillian Mlasani, aliishukuru BRELA kwa ufadhili huo na kuahidi baada ya kuhitimu watakuwa miongoni mwa wataalamu watakaojitoa kwa jamii ili elimu ya Miliki Ubunifu ifike mbali zaidi.

# Wanawake BRELA wajizolea sifa kwa uchapakazi

**Na Sheila Mfunami**

Watumishi wanawake wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), wamepongezwa kwa utendaji kazi mzuri na kutakiwa kuendelea kuzingatia sheria na kanuni za kazi na kuiwezesha Taasisi kufikia malengo yake.

Pongezi hizo zilitolewa tarehe 8 Machi, 2023 na Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa,

**"Kwanza niwapongeze wanawake wote kwa pamoja pia muongeze bidiii katika kutimiza majukumu yenu ikiwa ni pamoja na kuzingatia Maadili Sheria na Kanuni za kazi" alisema Bw. Nyaisa.**




*Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Bw. Godfrey Nyaisa (katikati) akishirikiana na watumishi wa BRELA Bi. Yvonne Maselle (kushoto) na Bi. Anna Nderingo (kulia), kukata keki ikiwa ni sehemu ya maadhimisho siku ya Wanawake Duniani.*

ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku wa Wanawake Duniani, katika ofisi za BRELA jijini Dar es Salaam.

Bw. Nyaisa aliwapongeza wanawake wa BRELA kwa kuendelea kutimiza majukumu yao kwa weledi wakati wote.

"Kwanza niwapongeze wanawake wote kwa pamoja pia muongeze bidiii katika kutimiza majukumu yenu ikiwa ni pamoja na kuzingatia Maadili Sheria na Kanuni za kazi" alisema Bw. Nyaisa.

"Wanawake mmekua chachu ya mafanikio makubwa, wengi wenu mnajitoa kwenye shughuli nyingi, mwanamke wa sasa sio kama wa kale, hivyo hongereni kwa kuwa mstari wa mbele kwenye kupambania maisha yenu na ninawatakia maadhimisho mema na maandamano yenye tija wanawake wote", alisisitiza Bw. Nyaisa.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu Bi. Loy Mhando, aliwapongeza wanawake kwa kujituma na kujitambua kwenye kutimiza majukumu yao ya kila siku.

Aidha Bi. Mhando aliwataka Wanawake wa BRELA kutokata tamaa mara wanapokumbana na changamoto zozote.

Wanawake wa BRELA baada ya kupata nasaha hizo walishiriki katika maandamano yaliyoandaliwa kimkoa katika Viwanja vya Mnazi Mmoja na badaye kupeleka mahitaji muhimu kwa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kituo cha kulea watoto yatima cha Maunga Center, kilichopo Kinondoni, jijini Dar es Salaam.

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake huadhimishwa tarehe 8 Machi kila mwaka duniani kote.




*Watumishi wanawake BRELA wakiwa katika picha ya pamoja siku ya maadhimisho ya Wanawake Duniani.*

# Tekelezeni kanuni za Wamiliki Manufaa - Homera

**Na Roida Andusamile**

Wamiliki wa Kampuni wametakiwa kutekeleza Kanuni za Wamiliki Manufaa wa Kampuni ili kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Homera, tarehe 29 Machi, 2023 katika hoteli ya Royal Tughimbe jijini Mbeya, wakati akifungua Warsha kuhusu utekelezaji wa Kanuni za Wamiliki Manufaa iliyowashirikisha Mawakili wa Kujitegemea, Washauri wa Biashara, Wafanyabiashara Watumishi wa Benki, Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu, ambazo zinawataka kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa wa Kampuni kwa Msajili wa Kampuni.

"Nimefahamishwa kuwa Kampuni nyingi bado hazijawasilisha taarifa hizo kwa Msajili wa Makampuni, inawezekana kuna changamoto katika uandaaji wa taarifa hizo na namna za kuziwasilisha Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), hivyo ni vyema mkatumia fursa hii kutatua changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa uwasilishaji wa taarifa hizi ambazo ni muhimu kwa mujibu wa sheria," amefafanua Mhe. Homera.

Awali akizungumza kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Mkuu wa Sehemu ya Kampuni




*Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Homera*

Bw. Isdor Nkindi alisema, mkoa wa Mbeya ni kati ya mikoa mitano iliyochaguliwa kutekeleza programu hiyo kutokana na takwimu nzuri ya mzunguko wa biashara na mwamko uliopo wa urasimishaji biashara.

Bw. Nkindi alisema BRELA pamoja na majadiliano na wadau wa biashara kuhusu utekelezaji wa Kanuni za Umiliki Manufaa, katika warsha hiyo washiriki watapatiwa nyenzo za kutumia wakati wa kuainisha Wamiliki Manufaa katika kampuni wanazozishauri na wanazoziendesha.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia muswada wa Sheria ya Fedha, ilipitisha marekebisho ya Sheria ya Kampuni Sura ya 212 kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa ambazo ni muhimu katika kuboresha mazingira ya uwekezaji, kikodi pamoja na kudhibiti utakatishaji wa Fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi.

Vilevile, mwaka 2021 Waziri mwenye dhamana alipitisha Kanuni za Umiliki Manufaa katika kampuni na kuanza kutumika rasmi mwaka 2022.



*Wadau wa BRELA wakifuatilia mada wakati wa mafunzo.*

# Watumishi BRELA wapigwa msasa

**Na Sheila Mfunami**

Watumishi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), wamepatiwa elimu kuhusu programu za Kompyuta (Software) inavyoweza kulindwa kisheria katika Hataza (Patent).

Akitoa elimu hiyo katika mafunzo yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Chuo cha Utumishi wa Umma jijini Dar es Salaam, Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma Mhe. Jaji Dkt. Adam Mambi alielezea kuhusu utaratibu wa kusajili programu za kompyuta kama Hataza.

Jaji Mambi alizungumzia pia kuhusu Sheria na Mikataba ya Kimataifa inayolinda Ubunifu katika programu za kompyuta ambayo itawezesha kurahisisha utoaji wa Hataza kwa waombaji.

"Tukatumie mafunzo haya kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza utumishi wetu na mkatoe elimu hii kwa watumishi wengine kila fursa ya kufanya hivyo inapopatikana", alisisitiza Jaji Mambi.

Alifafanua kuwa elimu hiyo itasaidia kujua namna ya kulinda haki za watu wanaobuni mifumo mbalimbali ya kiteknolojia.

Aidha, Jaji Mambi alisema mafunzo hayo yatasaidia kujua faida za kusajili majina ya biashara na kampuni kupitia mtandao, vilevile kujua sheria zinazosimamia matumizi ya huduma za kimtandao na usalama wa kimtandao.

"Washiriki wa mafunzo mkiwa kama wasaidizi wa Msajili katika utoaji wa huduma, mafunzo haya yatawasaidia kujua njia za kiusalama mtandaoni kama vile matumizi ya saini za kieletroniki na nywila (Password)," alifafanua Jaji Mambi.

Aidha, Jaji Mambi alisema mafunzo hayo yatasaidia kutatua changamoto za TEHAMA katika eneo Miliki Ubunifu (Intellectual Property).

**"Tukatumie mafunzo haya kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza utumishi wetu na mkatoe elimu hii kwa watumishi wengine kila fursa ya kufanya hivyo inapopatikana", alisisitiza Jaji Mambi.**



*Watumishi wa BRELA wakifuatilia uwasilishaji wa mada wakati wa mafunzo hayo.*

# BRELA kuchochea ujio wa wawekezaji nchini

**Na Peter Tweve**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), itaendelea kutoa elimu kuhusu dhana ya Wamiliki Manufaa wa Kampuni ili wawekezaji waendelee kuiamini nchi na kuendelea kuwekeza.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni na Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni na Majina ya Biashara kutoka BRELA, Bw. Meinrad Rweyemamu kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA wakati wa akifungua mafunzo ya siku mbili kuhusu dhana ya Wamiliki Manufaa kwa vyombo vya uchunguzi, yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Amboseli, Jijini Mwanza.

Bw. Rweyemamu alisema elimu hiyo kwa vyombo vya uchunguzi itasaidia kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa kusimamia sheria na kuweka mazingira mazuri ya biashara kwa wawekezaji.

"Hii itaisaidia nchi yetu kupata wawekezaji sahihi na wenye nia njema sio kufadhili ugaidi au mambo mengine yasiyofaa", alisema Bw. Rweyemamu.

Aliongeza kuwa katika kukabiliana na wimbi la utakatishaji fedha, ukwepaji kodi pamoja na ufadhili wa ugaidi unaofanywa na baadhi ya watu wasio waaminifu katika kampuni, BRELA inavishirikisha kwa pamoja vyombo vya Uchunguzi vilivyoidhinishwa kisheria katika upatikanaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa wa kampuni kwa kuwapatia elimu ya kudhibiti vitendo hivyo.

"Leo katika Ukumbi huu tumekutana na Maafisa kutoka Ofisi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Uhamiaji, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Vyombo hivi vimepewa mamlaka ya kisheria ya kupata taarifa kwaajili ya uchunguzi na uendeshaji wa mashtaka ya jinai yanayohusu kampuni, lengo ni kuziwezesha kampuni kuongeza uwajibikaji na uwazi katika shughuli zake" alisema Bw. Rweyemamu.

Kwa upande wake Mrakibu Msaidizi wa Uhamiaji Bw. Alfredy Mwenda alisema kupitia Sheria hiyo itawawezesha kutambua wamiliki halisi wa kampuni wenye hisa pamoja na Wakurugenzi na kutambua uraia pamoja na vibali vya kuishi na kufanya biashara nchini.



*Mshiriki wa mafunzo akichangia mada.*

Naye Afisa kutoka TAKUKURU, Bi. Dorothea Kinyonto alipongeza BRELA kwa mafunzo hayo kwani yanawaongezea ujuzi wa namna kuendesha shughuli zao za kufatilia mambo mbalimbali.

"Tunafuatilia mali za watuhumiwa pamoja na utakatishaji fedha katika kampuni mbalimbali, hivyo itatusaidia katika uchunguzi wetu unaohusu ukwepaji kodi kwa kuwafahamu wamiliki halisi wanaonufaika na kampuni", aliongeza Bi. Kinyonto.

Kwa upande wake Mrakibu Msaidizi wa uhamiaji Alfredy Mwenda kutoka Mwanza, alisema kupitia sheria hiyo itawawezesha kutambua wamiliki halisi wa Kampuni wenye hisa pamoja na wakurugenzi na kutambua uraia pamoja na vibali vya kuishi na kufanya biashara nchini.

BRELA inaendelea kuratibu na kutoa elimu wadau mbalimbali kuhusu masuala ya Miliki Manufaa ili Taifa liwe salama katika masuala ya utakatishaji fedha na kufadhili ugaidi.

Mpaka sasa mikoa minne kati ya mitano iliyopangwa kufikiwa imepata elimu hiyo, ambayo ni Dar es salaam, Dodoma, Arusha na Mwanza.



*Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni na Majina ya Biashara wa Bw. Meinrad Rweyemamu (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa mafunzo kuhusu Wamiliki Manufaa.*

# BRELA warudi darasani kutathmini wajibu wao

**Na Njwaba Mwaijibe**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeendesha mafunzo ya siku tano kwa watumishi wake kutoka Kurugenzi ya Kampuni na Majina ya Biashara ili kuwejengea uwezo na kuwaongezea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

Mafunzo hayo yalifanyika hivi karibuni katika ukumbi wa Wakala ya Mafunzo kwa njia ya Mtandao (TAGLA), jijini Dar es salaam, yakienda sambamba na kuwakutanisha na watalaamu kutoka kada nyingine ambao walibadilishana uzoefu.

Akizungumza katika ufunguzi wa mafunzo hayo Kaimu Mkurugenzi wa Kampuni na Majina ya Biashara Bw. Meinrad Rweyemamu alisema kuwa mafunzo hayo yameratibiwa kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kutambua changamoto za wadau wanapo hitaji huduma za BRELA.

"Mafunzo haya ni muhimu katika kuboresha namna ya Utendaji kazi, hivyo ni vyema kila mmoja kuzingatia kuanzia mwanzo mpaka mwisho kwani tutapitia baadhi ya vipengele katika sheria ya Kampuni na kuona vile tunavyovitekeleza na jinsi wadau wanavyotupokea nje, yatakuwa mafunzo yenye majadiliano zaidi. Mkumbuke Msajili ndiye anatunza taarifa za Kampuni zote kwa hiyo tutakuwa na mada tofauti ambazo zitawaongezea ujuzi na mfahamu huko nje wanatafsiri vipi sheria hizi", alisema Bw. Rweyemamu

Sambamba na hayo alizitaja faida mbalimbali za kuandaa mafunzo kama hayo ikiwa ni pamoja na kufahamu kipi wateja wa nje wanakumbana nacho na kuona namna ya kuongeza utendaji kwa watumishi wa idara yake na kuzitatua changamoto za wadau kwa wakati.

Akiwasilisha mada kuhusu maswala ya Ufilisi katika Mafunzo hayo, Wakili wa Kujitegemea Bw. Charles Rwechungura alifafanua kwa kina kuhusu sheria ya Makampuni kwa upande wa Ufilisi, na hatua za usajili wa Mikopo.

Aliwakumbusha watumishi kuhakikisha wanazingatia kuhakiki nyaraka mbalimbali kwa umakini ambazo zinatakiwa na msajili wakati wa usajili wa mikopo huku akichangia uzoefu wake katika masuala ya ufilisi wa Kampuni na namna ambavyo sheria inataka ili kuhakikisha Kampuni ambazo zimeanzishwa zinakidhi matakwa yake.

Msajili ni mtekelezaji wa Sheria ya Kampuni Sura 212, hivyo elimu hii itawasadia kuongeza uelewa na namna taratibu za ufilisi/uokozi wa Kampuni zinafanyika kabla nyaraka zake kuwasilishwa kwa msajili pia imewaongezea maarifa ya namna ya kuwashauri wateja kwenye masuala yahusuyo Kampuni.




*Watumishi wa BRELA wakifuatilia mafunzo kwa umakini.*

# BRELA yawakumbusha wafanyabiashara kusajili, kutumia nembo



*Baadhi ya washiriki wakifuatilia mafunzo.*

**Na Sheila Mfunami**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imewakumbusha Wamiliki wa Viwanda na Wafanyabiashara kusajili na kutumia nembo zao katika bidhaa ili ziweze kuwanufaisha.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni kwenye Warsha iliyoandaliwa na Taasisi hiyo katika ukumbi wa Chuo cha Utalii, Jijini Dar es salaam.

Akifungua warsha hiyo aliyekuwa Kaimu Mkurugenzi wa Miliki Ubunifu kutoka BRELA, Bw. Seka Kasera alisema lengo la kukutana na wadau hao muhimu ni kuendelea kuwakumbusha wajibu wao wa kulinda na kukuza bunifu nchini.

"Leo tumekutana na wafanyabiashara kwa lengo la kuwakumbusha kuhusu masuala ya Miliki Ubunifu hasa Alama za Biashara na Huduma (Nembo) na Hataza, ambazo ni huduma zinazotolewa na BRELA.

Ni matarajio yetu kwamba baada ya warsha hii wadau hawa watakuwa na uelewa mpana kuhusu masuala yanayohusu huduma hizo na jinsi ya kutumia katika biashara zao ili kukuza uchumi" alieleza Bw. Kasera.

Aliongeza kuwa ubunifu katika karne hii ya sayansi na teknolojia umekuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi hivyo wamiliki na wafanyabiashara hawana budi kutumia bunifu zao ili kujikuza zaidi.

Bw. Kasera alizitaja faida za kutumia nembo iliyosajiliwa katika bidhaa kuwa ni pamoja na kumpa mfanyabiashara haki ya kipekee kutumia alama husika na kuwazuia wengine kutumia alama hiyo isipokuwa kwa ruhusa au ridhaa yake.

Faida nyingine ni kudhibiti ushindani wa bidhaa au huduma katika soko, kuendeleza umaarufu wa ubora wa bidhaa au huduma, kuhifadhi ulinzi wa alama iliyosajiliwa pamoja na mabadiliko husika.

Pia kumpatia mmiliki wa Alama husika kipato kwa njia ya kuuza Alama au kutoa haki ya matumizi kwa mtu mwingine.

Alitaja faida nyingine kuwa ni kuwawezesha watumiaji wa bidhaa kutambua na kuchagua alama au huduma kutokana na ubora na kumpa mmiliki haki ya kisheria kumchukulia hatua mtu anayeiga alama hiyo.

Naye aliyekuwa Afisa Mwandamizi kutoka Idara ya Miliki Ubunifu BRELA, Bw. Raphael Mtalima aliwaeleza wadau kuhusu Hataza ambayo ni hati inayotolewa na Serikali kwa mvumbuzi kutokana na uvumbuzi alioufanya wa kitu au namna ya kuunda kitu unaolenga kutatua tatizo au kutoa jawabu/ ufumbuzi mahsusi katika nyanja ya teknolojia husika.

Aliongeza kuwa Ili uvumbuzi upatiwe Hataza unatakiwa uwe mpya, uoneshe njia ya uvumbuzi na pia uweze kutumika katika eneo husika na usajili wake unafanyika kwa njia ya mtandao.

BRELA inaendelea na utaratibu wake wa kutoa elimu ya Miliki Ubunifu katika sehemu mbalimbali kwa kuandaa warsha na makongamano mbalimbali ili wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo wanufaike na elimu hiyo.

# Bodi ya ushauri BRELA yawataka wanawake viongozi kujituma

**Na Sheila Mfunami**

Watumishi wanawake viongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), wametakiwa kuzingatia mambo ya msingi katika utendaji kazi ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Rai hiyo ilitolewa hivi karibuni na Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya BRELA, Prof. Neema Mori, wakati ya mafunzo maalum ya uongozi kwa watumishi wanawake viongozi wa Taasisi hiyo katika hoteli ya Hyatt, jijini Dar es Salaam.

Prof. Mori aliyataja mambo ya msingi anayopaswa kuyazingatia kiongozi kuwa ni nidhamu, utii, bidii, kujituma, pamoja na mawasiliano mazuri na wengine.

"Kama viongozi mkiyazingatia haya mtafanya maamuzi sahihi yenye kuleta tija ", alieleza Prof. Mori.

Prof. Mori alieleza pia kuwa viongozi wanawake wanapaswa kujitambua na kuziishi ndoto zao kwa kutekeleza majukumu yao na kufikia malengo waliyojiwekea.

"Kila mwanamke ni kiongozi katika nyanja tofauti, hivyo ni vyema kufahamu nafasi yako mahali ulipo, hii itasaidia kujiongoza na kuwaongoza wengine", alisisitiza Prof. Mori.

Alisema mafunzo hayo maalum yamelenga katika kupeana elimu na kujadiliana juu ya masuala muhimu ya kuzingatia kama viongozi na namna mwanamke anavyoweza kuwa kiongozi hodari na mwenye kufanya majukumu yake pasipo kuwa na uoga wowote.




*Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri wa BRELA Prof. Neema Mori*

Prof. Mori alifafanua kuwa suala la nidhamu, kuishi kwa usawa na kufanya matendo yenye kuongeza tija katika jamii kama viongozi yatawafanya wakumbukwe na wengine kufuata nyayo zao.

Aliongeza kuwa ni vema kutambua aina ya watu wanaowaongoza kwani kuna watu wenye tabia zinazotofautia ambazo wakati mwingine huleta ugumu katika uongozi hivyo, mnapaswa kujua ni jinsi gani mnaweza kusaidiana.

Mafunzo haya ya siku moja yaliandaliwa na Prof. Mori kwa kushirikiana na uongozi wa Taasisi kwa lengo la kuwajengea uwezo wanawake.



*Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya BRELA Prof. Neema Mori (aliyeketi katikati), akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wanawake viongozi wa BRELA. Aliyeketi kulia ni Mjumbe wa Bodi ya Ushauri Bi. Judith Kadege*

# BRELA yakutana na wadau wa sekta binafsi

**Na Theresa Chilambo**



*Wadau kutoka sekta binafsi wakifuatilia mada wakati wa mafunzo.*

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imekutana na wadau wa sekta binafsi na kuwajengea uwezo kuhusu dhana ya Kanuni za Wamiliki Manufaa wa Kampuni zinazomilikiwa na Wabia kwa lengo la kuelekezana mabadiliko ya sheria na kupokea uzoefu kutoka kwa wabobezi wa masuala ya sheria na biashara.

Akifungua warsha ya siku moja katika ukumbi wa Ngorongoro Jijini Arusha, hivi karibuni kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA Kaimu Mkuu wa Sehemu ya Makampuni, Bw. Isidory Nkindi, alieleza kuwa Kanuni za Wamiliki Manufaa zinataka Kampuni kuwasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa wa mwisho katika Kampuni.

Alieleza kuwa Wamiliki Manufaa ni wale wenye manufaa kwenye kampuni kwa kumiliki hisa, haki ya kupiga kura na kutoa maamuzi kwenye uendeshaji wa kampuni.

"Kama mnavyojua, Bunge la Jamhuri Muungano wa Tanzania kupitia Mswada wa Sheria ya Fedha, ya mwaka 2020, lilipitisha marekebisho ya Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa taarifa za Wamiliki Manufaa (beneficial owners) katika kampuni ambazo ni muhimu katika kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara, sababu za kikodi pamoja na kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi", alifafanua Bw. Nkindi.

Pia alisema kupitia majadiliano haya, BRELA inatarajia kuwa na mjadala mpana wenye lengo la kuboresha hasa kwenye maeneo ya "Substantial Control" na kampuni za kigeni ambayo yameanza kuleta tafsiri kinzani.

"Ni matarajio ya Taasisi kuwa elimu hii itawawezesha kuwa mabalozi wazuri katika utekelezaji wa sheria kwa kuwa mnawahudumia wenye Kampuni, hivyo ni vema mkatoa ushauri kwa usahihi", alisisitiza Bw. Nkindi.

Kwa upande wake, wakili wa kujitegemea kutoka Chama cha Mawakili, Bi. Fauzia Mustapha alihitimisha kwa kusema kuwa warsha hiyo imekuwa ya manufaa kwakuwa kanuni hizo ni mpya hivyo watafahamu kwa undani kuhusu dhana nzima na namna ya kuwasilisha taarifa kwenye mfumo pamoja na kushauri maboresha kwenye kanuni zilizopitishwa ili kuwa rafiki katika kuhudumia umma.

Wadau walioshiriki warsha hiyo ni wafanyabiashara, taasisi za fedha, wanasheria, wahasibu, waliosajiliwa kusaidia Kampuni kwenye masuala ya ushauri, kisheria na kimahesabu.



*Wadau kutoka sekta binafsi wakifuatilia mada wakati wa mafunzo.*

# Urasimishaji biashara waongezeka miaka miwili ya Rais Samia



**Na Nehemia Mihayo**

Tanzania kwa mara ya kwanza tarehe 19 Machi, 2021, iliandika historia mpya ya kuwa na Rais Mwanamke aliyeingia madarakani kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, ambaye si mwingine bali ni Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tarehe 6 Aprili, 2021 Rais Samia Suluhu Hassan anatambulisha salamu mpya ambayo imejaa matumaini makubwa na kuitia hamasa ya kuendelea mbele na kuinyanyua Tanzania na kuiweka katika ramani ya Dunia. Salamu hiyo iliyotambulishwa inasema "Jamhuri ya Muungano wa Tanzania" na kila mtu anapaswa kuitikia "kazi iendelee".

Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ametimiza miaka miwili ya kuwa madarakani tarehe 19 Machi, 2023. Katika kipindi cha Miaka miwili ya uongozi wake, Uwekezaji na Nyanja ya biashara imeendelea kukua na kuimarika kila siku.

Katika kuunga mkono Jitihada za Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), imeendelea Kuweka mazingira wezeshi ya biashara nchini kwa kurasimisha biashara na kulinda miliki-ubunifu kupitia sajili, utoaji wa leseni na udhibiti wa mwenendo wa biashara.

Afisa Mtendaji Mkuu wa BRELA, Bw.Godfrey Nyaisa ameeleza kuwa lengo kuu la Taasisi anayoiongoza ni kutengeneza mazingira rafiki na wezeshi sio tu kwa wawekezaji bali wafanyabiashara wote.

Katika kutekeleza hilo, kila mtumishi ndani ya Taasisi anajengewa uwezo kufahamu dira, dhima na misingi ya Taasisi ili kuwa na uwezo wa kuwahudumia wananchi kwa kiwango cha hali ya juu ili wapate hamasa ya kurasimisha biashara zao na hatimaye kuchangia katika kutekeleza malengo, mipango na mikakati ya maendeleo ya Taifa.

Ameeleza Bw. Nyaisa kuwa Mwezi Desemba, 2021 BRELA ilizindua rasmi Mkataba wake wa Huduma kwa Mteja. Lengo likiwa ni kujenga uelewa kwa Wateja kuhusu upatikanaji wa huduma, viwango vya ubora wa huduma hizo na matarajio ya Wateja kwa Wakala.

Katika Mkataba huo, imewekwa bayana kuwa muda wa usajili wa Jina la biashara ni siku moja (1) na si zaidi ya siku tatu (3) za kazi, Usajili wa kampuni ni siku tatu (3) na si zaidi ya siku tano (5) za kazi. Usajili wa Alama za Biashara na huduma ni kipindi cha siku tisini (90) (kutokana na takwa la kisheria), maombi ya kupata Hataza ni siku mia moja na ishirini (120) (kutokana na takwa la kisheria), kupata Leseni ya Kiwanda au Leseni ya Biashara kundi "A" ni siku moja (1) na si zaidi ya siku tatu (3) za kazi.

" Mkataba wa Huduma kwa Mteja unadhihirisha wazi kuwa BRELA imedhamiria kwa dhati kumhudumia mteja bila usumbufu wowote hivyo wafanyabiashara wasisite kutumia huduma zinazotolewa na BRELA wakatis wote", anafafanua Bw. Nyaisa.

Anaeleza kuwa, BRELA imeendelea kufanya maboresho ya mifumo yake ya Sajili na Leseni na marekebisho ya Sheria inazozisimamia ili ziendane na mazingira ya biashara ya wakati huu, ukuaji wa Teknolojia, utoaji wa huduma wa haraka na malengo ya Serikali ya Awamu ya sita ya utoaji wa huduma kwa wananchi kwa haraka na bila vikwazo.

Juhudi hizi zimepelekea BRELA kupata mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka miwili chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwani mwenendo unaonesha kuwa katika kipindi cha miezi 12. kuanzia Januari hadi Desemba 2021 Kampuni za ndani zilizosajiliwa ni 10,790 ikilinganishwa na Kampuni 13,663 zilizosajiliwa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2022.



***Watumishi wa BRELA wakiwa katika picha ya pamoja na watumishi***

Katika kipindi hicho ongezeko la Kampuni 2,873 ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 27 limechochewa na mazingira mazuri ya biashara yanayoendelea kuimarika kila siku. Kwa upande wa Kampuni za Kigeni katika kipindi cha miaka miwili zimeongezeka kwa asilimia 29 kwa kuangalia mwenendo wa mwaka 2021 kwenye kipindi cha miezi 12 kuanzia Januari hadi Desemba ambapo zilisajiliwa Kampuni za Kigeni 72 huku kampuni 93 zikisajiliwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

BRELA katika kipindi cha miaka miwili ya 2021 na 2022 kimenukuu ongezeko la asilimia 17 katika Usajili wa Majina ya Biashara. Katika kipindi tajwa mwaka 2021 Majina ya Biashara yaliyosajiliwa yalikuwa ni 21,836 ukilinganisha na 25,507 yaliyosajiliwa kwa kipindi hicho hicho mwaka 2022. Bw. Meinrad Rweyemamu ni Kaimu Mkurugenzi wa Makampuni na Majina ya Biashara kutoka BRELA ambaye anaeleza kuwa lengo la taasisi ni kulea biashara na kuhakikisha zinastawi na kuwa na mwendelezo. "BRELA inajukumu la kulea hizi biashara ili zisiweze kudhoofika kutokana na hali hiyo tumekuwa tukitumia njia mbalimbali za kuhakikisha kwamba changamoto zilizo ndani ya majukumu ya Wakala zote tunaziondoa" ameeleza Bw. Rweyemamu.

Pia ameongeza kuwa BRELA imekuwa na utaratibu wa kutatua migogoro baina ya Wamiliki wa biashara ambao wamerasimisha biashara zao kwa mujibu wa sheria. Migogoro hiyo mingi imekuwa ikidhoofisha ukuaji wa biashara hizo. Mwaka 2022 BRELA iliandaa zoezi maalum la kutatua migogoro ya aina hii ili kuhakikisha kuwa biashara zinaepukana na changamoto hii. Zoezi hili lilipewa Jina la "Suluhisha na BRELA" ambalo ilifanyika kuanzia Juni 13 hadi 19, 2022 ambalo lilitekelezwa kwenye kumbi zilizopo ndani ya Makumbusho ya Taifa Jijini Dar es Salaam.

Kwa upande wa Sajili za Alama za Biashara na Huduma Wakala imenukuu ongezeko la asilimia kumi na tano katika sajili hizo kwa kulinganisha miaka miwili ya 2021 na 2022 kwa kipindi cha miezi kumi na mbili kuanzia Januari hadi Desemba.

Katika kipindi tajwa mwaka 2021 Wakala ilisajili 3,137 ikilinganishwa na 3,607 katika kipindi kama hicho. Kwa upande wa Leseni za Biashara kundi "A" ongezeko la Leseni 1689 limenukuliwa kutokana na ulinganifu wa leseni zilizotolewa mwezi Januari hadi Desemba 2021 zikiwa ni 12,574 ukilinganishwa na 14,263 katika kipindi kama hicho. Mkurugenzi wa Leseni kutoka BRELA, Bw. Andrew Mkapa amebainisha kuwa ongezeko hili limechochewa na jitihada mbalimbali ikiwemo kuwajengea uwezo Maafisa biashara katika kuwawezesha wamiliki wa biashara ndogo na za kati kuzilea na kuzikuza.

Kutokana na dhima hiyo BRELA inatekeleza mpango maalum wa kuwajengea uwezo Maafisa Biashara na TEHAMA katika Mikoa yote ya Tanzania bara. Mpaka sasa Wakala imetekeleza lengo hilo kwa kutoa mafunzo kwa Maafisa biashara wa Mikoa 19 ambayo ni Tabora, Kigoma, Katavi, Shinyanga, Pwani, Dar es salaam, Lindi, Mtwara, Singida, Dodoma, Morogoro, Mwanza, Geita, Mara, Kagera, Rukwa, Songwe, Lindi na Mtwara.

Aidha, ameeleza kuwa BRELA imekuwa na utaratibu wa kuwatembelea wafanyabiashara katika maeneo yao kwa ajili ya kutambua changamoto wanazokutana nazo, kuwapa elimu kuhusu faida za urasimishaji biashara na kuwahamasisha kufanya sajili. Mpaka sasa Wakala imeweza kuwatembelea na kuwafikia wamiliki wa viwanda katika Dodoma, Morogoro, Katavi, Pwani, Kilimanjaro, Kagera, Rukwa na Dar es Salaam. Pia Wakala umefanya ukaguzi elimishi wa Leseni za Biashara Kundi "A" katika Mikoa nane (8) ya Tanzania bara ambayo ni Dodoma, Morogoro, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kagera Shinyanga, Tanga na Mwanza.

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

# A CALL FOR COMPANIES TO FILE ANNUAL RETURNS

The Registrar of Companies calls all companies incorporated and registered in Tanzania to file their annual returns/financial statements as required by the Companies Act, CAP 212.

**HOW TO FILE ANNUAL RETURNS & FINANCIAL STATEMENTS THROUGH THE ONLINE REGISTRATION SYSTEM**

1. Log in on the Online Registration System (ORS).
2. Select 'e - service'.
3. Select 'Company' .
4. Select 'Filing of annual return (accounts) / Update.'
5. Fill in Incorporation/Compliance number.
6. Fill in company's details.
7. Upload form 128 together with a signed and dated consolidated form.
8. Select mode of payment (Mobile or Bank).
9. After payment the application will be received for review.

**Note:** Filing fee of an annual return is Tzs. 22,000 / - if submitted on time. Delayed submission of an annual return attracts a late filing fee of Tzs. 2500 / - (compounded) per every delayed month or part thereof.

**BRELA HOUSE**
Plot No 23, Block No. 20,
Sokoine Drive/Shaaban Robert Street,
P.O Box. 9393, 11101
Ilala, Dar es Salaam.

**DODOMA OFFICE**
PSSF Building
Makole Street 10th Floor

*"We give legal life to your business"*

Telephone:+ 255 22 2212800, E-mail: ceo@brela.go.tz, usajili@brela.go.tz,
Website: www.brela.go.tz




BRELA tanzania | Brela _tanzania | brela _tanzania | brela _tanzania